KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA KILICHOKETI KUJADILI MREJESHO WA UJENZI WA MADARASA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 27/10/2021.

WATAALAMU WALIOHUDHURIA.

1. Mwantum Mgonja- Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Frank E. Komba -Afisa Rasilimali Watu (W)
3. Veronica Kinyemi - Katibu Tawala (W)
4. Benjamin B. Majoya - Afisa Elimu Sekondari (W)
5. Kaunga Amani - Afisa Mipango (W)
6. Jumanne U. Mtinangi -Mwanasheria (W)
7. Kokuhumbya Mishako -Afisa TEHAMA (W)
8. Faidha S. Kassim -Mkaguzi wa Ndani (W)
9. Peter Nambunga -Afisa Maendeleo Jamii (W)
10. Salon Nyika -Mweka Hazina (W)
11. Beda Mbaga -HPMU
12. Shaidu R. Mudrica -Kaimu Mhandisi Ujenzi (W)
13. Zawadi S. Kalugira -Mhasibu Mapato
14. Cleophas Murugwa-Kaimu Afisa Mazingira (W)
15. Salum Mwamfula -Afisa Uchaguzi (W)
16. Julita E. Bulali -Afisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji (W)
17. Anna Kiria -Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
18. Eliashukura Tito -Mratibu Uthibiti Ubora (W)
19. Michael Mpupua -Afisa Biashara
20. Angelus R. Mtewa -Kaimu Mganga Mkuu (W)
21. Safina Msemo -Mratibu TASAF
22. Jessy Mpangala -Afisaelimu Msingi (W)
23. Mary Gwabila -Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W)

WATAALAMU AMBAO HAWAKUHUDHURIA.

J.D Swai -Mratibu Udhibiti Ukimwi (W)

.................................... 
SAINI YA KATIBU
TAREHE 6/6/2022

....................................
SAINI YA MWENYEKITI
TAREHE 6/6/2022

CamScanner

**SEKERETARIETI**

1. P.G.Lukindo -Mwandishi wa Mikutano.
2. Revocatus Ishengoma -Mwandishi wa Mikutano.
3. Sharen Mkani -Mwandishi wa Mikutano.

**ORODHA YA AGENDA.**

1. Kufungua Kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Mrejeshowa mgawanyo wa vyumba vya Madarasa.
4. orodha ya vikundi vilivyopendekezwa kupata mikopo mwaka wa fedha 2021/2022 awamu ya kwanza.
5. Kufunga Kikao.

**MUHT.NA.5/MKR/FUM/OKT/40/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO**

40:01 Kabla ya kufungua kikao Katibu aliwaeleza wajumbe kwamba kikao kile kilikuwa ni kikao maalum cha kujadili mrejesho wa mgawanyo wa vyumba vya madarasa.Kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili afunguekikao.

40:02 Mwenyekiti alimshukuru Mungu kwa nafasi ile na aliwaeleza wajumbe kwamba kikao kile kilikuwakinategemewa kujadili agenda ya mgawanyo wa madarasa naorodha ya vikundi vilivyopendekezwa kupata mikopo mwaka wa fedha 2021/2022 awamu ya kwanza.Alifungua kikao saa02:35asubuhi.

**MUHT.NA.5/MKR/FUM/OKT/41/2021/2022:KURIDHIA AGENDA.**

41:01 Katibu aliwasilisha agenda 5 ili ziweze kujadiliwa.

41:02 Wajumbe waliridhia kujadili agenda 5 kamazilivyowasilishwa.

**MUHT.NA.5/MKR/FUM/SEPT/42/2021/2022MREJESHO WA MGAWANYO WA VYUMBA VYA MADARASA.**

42:01 Katibu aliwasilisha agenda ya mrejesho wa mgawanyo wa vyumba vya madarasa.

42:02 Taarifa ilionesha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga imepokea jumla ya 3,090,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 116, kwa ajili ya kuwezesha wanafunzi wa kidato cha kwanza 2022, ambao wataanza kujiunga na kidato cha kwanza kwamwaka huo. Wajumbe walisomewa taratibu zote ikiwemo utaratibu wa manunuzi ambapo ni manunuzi yanatarajiwa kuwa ni manunuzi ya jumla.

SAINI YA KATIBU

TAREHE 06/06/2022

SAINI YA MWENYEKITI

TAREHE 06/06/2022

42:03Wajumbe waliipokea na kuijadili.

42:04Wajumbe walimpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wake katika suala la ujezi wa vyumba vya madarasa. Wajumbe wakijadili waliona kwamba nivema mafundi wote kwapamoja wakaitwa ili wapate maelekezo yataratibu zinazotakiwa kutumiwa wakatiwa ujenzi na pia kuzingatia muda.

42:05 Kuhusu mapendekezo yaliyokuwepo ya kutumia jeshi la akiba, wajumbe walikubaliana kwamba ni vema kutumia wananchi waliopo katika maeneo husika kama vibarua, kwani wanaouzoefu wa kutosha, katika kazi hizo badala ya jeshi la akiba.

42:06Aidha wajumbe walielezwa kwamba kwa upande wa mabweni kigezo kilichozingatiwa kilikuwa ni pamoja na umbali kutoka wanapoishi watoto, mahitaji maalum.

42:07Wajumbe walielezwa mikakakati kwajumla usimamizi ngazi ya tarafa walishuriwakufikisha taaraifa ya ujenzi huo ngazi ya kamatiza maendeleo za kata.

42:08Wajumbe waliipitisha agenda ya mrejesho wa mgawanyo wa vyumba vya madarasa.

**MUHT.NA.5/MKR/FUM/SEPT/44/2020/2021:KUFUNGA KIKAO.**

44:01 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao.

44:02 Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti. Aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano wao.. Alifunga kikao saa 03:45 alasiri.

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ……………………………… | ……………………………… |
| **SAINI YA KATIBU** | **SAINI YA MWENYEKITI** |
| SALUM M. MWAMFULA | MWANTUM H. MGONJA |
| **JINA LA KATIBU** | **JINA LA MWENYEKITI** |
| **TAREHE**..6.|.6.|.2022.... | **TAREHE**..6.|.6.|.2022.... |